HABARI LEO UK 8.

# Uzalishaji vifaranga vya samaki kuongezeka

Na John Nditi, Morogoro

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema itaendeleza mikakati na jitihada mbalimbali katika kuhakikisha inazalisha vifaranga vya samaki kwa wingi.

Imesema hilo litakwenda sambamba na kutoa elimu ya ufugaji wa vifaranga kwa wananchi ili waweze kujiongezea kipato na kukuza uchumi wa taifa.

Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji wa Wizara hiyo, Dk Nazael Madala alisema hayo juzi mjini Morogoro kabla ya kumkaribisha Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji Mali wa mkoa huo, Dk Rozalia Rwegasira kufungua mafunzo rejea kwa maofisa ugani wa kutoka halmashauri za mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Pwani na Kilimanjaro.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Kituo cha Uzalishaji wa vifaranga vya samaki Kingolwira kilichopo Manispaa ya Morogoro ambayo yalilenga kuhamasisha, kuendeleza, kusimamia tasnia ya ukuzaji viumbe maji na kuzalisha kwa tija.

Madala alisema uzalishaji wa vifaranga vya samaki katika mwaka wa fedha 2020/2021, vituo vitatu viliweza kuzalisha 1,901,717.

Alisema kwa kutambua jukumu hilo, wizara imeweka mkakati wa uzalishaji kwa wingi wa vifaranga vya samaki katika vituo vyake vitano vilivyopo nchini.

Alivitaja vituo vitatu vinavyozalisha vifaranga kwa sasa kuwa ni Ruhila (Ruvuma), Mwanapuli (Tabora) na Kingolwira cha Morogoro.

"Uzalishaji wa vifaranga vya samaki kwa mwaka 2020/2021 vituo hivyo vitatu viliweza kuzalisha vifaranga vya samaki 1,901,717. Ruhila kilizalisha 972,305, Mwanapuli 457,812 na Kingolwira vifaranga 471,600," alisema.

Alisema wizara kwa sasa imejipanga kuhakikisha ufugaji wa samaki unakuwa endelevu na wenye kuleta tija kwa wafugaji sambamba na utoaji elimu sahihi ya ufugaji wa samaki.

"Kutokana na juhudi zinazofanywa na wizara hii ninawahimiza Watanzania wajitokeze kufuga samaki na viumbe maji wengine ili kujiongezea kipato chao na Taifa kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji Mali, Mkoa wa Morogoro, Rwegasira aliwashauri Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo katika uchumi wa buluu kutokana na kuwepo rasilimali maji ikiwemo bahari, maziwa, mito na maeneo oevu ambayo yanatoa wigo mpana wa kufanya shughuli za ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa majini.

Rwegasira alisema licha ya serikali kuwekeza rasilimali nyingi katika sekta ya mifugo na uvuvi, bado uzalishaji wa mazao ya viumbe maji ni mdogo ukilinganisha na fursa zilizopo nchini.

Scanned with CamScanner

na

)

›o kuanzia
ıadi
›ata tuzo
ıtika na-
huduma
ıawake
ı watoto
za Mkoa
aam,"

de wake,
ıu wa
.mana am-
‹ua nafasi
›, alisema
ıendeleza
ambayo
a aliyem-
ıye pia
vake.
:isha
huduma
ɜja kwa
diyo
ıduma za
ni kuwa
ı.



Sh
jo,
MB).

# Wadau sekta ya uvuvi waanza mafunzo muhimu

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), imeanza kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali waliopo katika sekta hiyo yenye lengo la kuwapa elimu kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa hiari wa kitaifa wa kuendeleza uvuvi mdogo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa warsha iliyowahusisha wadau kutoka katika taasisi za serikali, mashirika binafsi, Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo (FAO) na baadhi ya halmashauri zenye shughuli za uvuvi, Katibu Mkuu Sekta ya Uvuvi, Amos Machilika aliwataka wadau hao kuzingatia mafunzo hayo kutokana na umuhimu wake.

Machilika ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema uanzishwaji wa mpango huo ni hatua mojawapo ya serikali ya kuendelea kuwajali wavuvi wadogo kwa kuanzisha mradi wa kupunguza umasikini na kuongeza usalama wa chakula na lishe unaozingatia usawa wa kijinsia.

Alisema katika kutekeleza mwongozo huo wa hiari wa kuendeleza uvuvi mdogo uliopitishwa na wadau wote waliopo katika mnyororo wa sekta hiyo ni muhimu kila mdau kwa nafasi yake kuhakikisha anatimiza wajibu wake ili utekelezaji uweze kuleta tija.

Machilika alisema kupitia mradi huo mpya unaotekelezwa kwa miaka miwili, matarajio ya serikali ni kupunguza umasikini, kuboresha lishe na kipato kupitia shughuli zinazofanyika kutokana na mnyororo wa thamani wa mazao yatokanayo na uvuvi mdogo.

Mwakilishi wa FAO kwa upande wa sekta ya uvuvi, Dk Oliva Mkumbo alisema Tanzania ndio nchi ya kwanza kuandaa mpango kazi wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa hiari.

Aliipongeza Serikali kwa kuendelea kuwajali wanawake wanaojishughulisha na uvuvi mdogo ikiwa ni pamoja na Jukwaa lao la TAWFA.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uvuvi, Didas Mtambalike alisema mradi huo utaanza kutekelezwa katika halmashauri tano za Kilwa, Pangani, Mwanga, Kigoma na Ilemela.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi, Fatma Sobo mbali na kuishukuru serikali kwa kuendelea kuwajali wavuvi wadogo pia alipongeza uanzishwaji wa mradi huo kwa kuwa utasaidia sana katika kupunguza umasikini, kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora pamoja na kuwaongezea kipato wavuvi wadogo.

Scanned with CamScanner

Katura alisema tayari wakazi wa kijiji hicho wamechanga zaidi ya Sh11 milioni kutekeleza mradi

wazito na watoto ambao ndio waathirika wa kukosekana kituo cha afya katika kata hiyo.

Mwenyekiti kijiji cha Kamara, Omary Katura

utawapunguzia adha wananchi," alisema Dk Lusajo.

MWANANCHI UK 20.

# Samaki waadimika, bei yapaa

Saada Amir, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz



**Sh5,000**

Kiwango cha fedha kilichoongezeka katika bei ya samaki kulingana na ukubwa wake.

**Sh8,000**

Bei ya samaki ya sasa ambaye awali aliuzwa Sh5,000.

**Mwanza.** Wakazi wa jijini Mwanza na vitongoji vyake walio-zoea kitoweo cha samaki inabidi 'watoboke' zaidi mifukoni au kutafuta vitoweo vingine kutokana na samaki kuadimika na hivyo kusababisha bei kupaa sokoni.

Ingawa bei imepanda kwa aina zote za samaki, walaji na wapenzi wa samaki aina ya sato ndio wameathirika zaidi baada ya bei ya kitoweo hicho kupanda kwa wastani wa kati ya Sh3,000 hadi Sh5,000 kulingana na ukubwa.

Uchunguzi uliofanywa na *Mwananchi* katika soko la Mkuyuni, Mbugani, Igogo na Soko Kuu jijini Mwanza umebaini samaki aina ya sato mwenye ukubwa unaoweza kukatwa vipande vitatu au vinne ambao awali waliuzwa Sh3,000 hadi Sh4,000, sasa wanauzwa kati ya Sh6,000 hadi Sh6,500.

Samaki waliokuwa wakiuzwa Sh5,000 sasa wanauzwa Sh8,000 wakati waliokuwa wakiuzwa Sh10,000 sasa wanapatikana kwa Sh15,000.

Akizungumza na *Mwananchi* kwa njia ya simu kuhusu kuadimika na ongezeko la bei ya samaki, Mwenyekiti wa chama cha wavuvi Tanzania (Tafu), Bakari Kadabi alisema hali hiyo imetokana na kupungua kwa wafanyabiashara wadogo wanaolangua bidhaa hiyo na kuifikisha sokoni kwa walaji.

"Mnyororo wa biashara ya samaki unaohusisha wavuvi aina tatu za washiriki; wapo wavuvi, wafanyabiashara wakubwa, wa kati, walanguzi ambao ndio hufikisha bidhaa sokoni. Idadi ya walanguzi ambao ni kiungo muhimu kimepungua katika siku za hivi karibuni baada ya machinga kuondolewa mitaani," alisema Bakari.

Akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina wala kiwanda chake, Ofisa biashara na mauzo wa moja ya viwanda vya kuchakata mazao ya samaki jijini Mwanza alithibitisha ongezeko la malighafi na kushuka kwa bei ya kununulia samaki kutoka kwa wafanyabiashara wa kati.

"Tunapata malighafi ya kutosha. Hata magari yetu yanayokusanya samaki kutoka mialo ya uvuvi hivi sasa inapata malighafi kwa muda mfupi tofauti na siku za nyuma; hii imetupa si tu uhakika wa malighafi, bali pia unafuu katika bei," alisema ofisa huyo. Hata hivyo, muuza samaki katika soko la Mbugani, Ashura Suleiman alisema walazimika kuongeza bei kumudu gharama na mahitaji ya soko. "Wafanyabiashara wa kati wanaonunua samaki kutoka kwa wavuvi wametupandishia bei, hivyo nasi ni lazima tuongeze kidogo kuokoa mitaji na kupata faida kidogo," alisema. Magreth Yohana, mteja aliyekutwa soko la Mkuyuni alisema sasa familia yake imetumia vitoweo vingine ikiwemo nyama, dagaa na samaki wadogo maarufu kama furu pamoja na mboga za majani.

Scanned with CamScanner

UHALIFU

# Ng'ombe 16 wafa maji Kilosa

Juma Mtanda, Mwananchi
jmtanda@mwananchi.co.tz

**Morogoro**. Ng'ombe 16 kati ya 84 wanaodaiwa kuporwa wakiwa malishoni wamekufa maji walipokuwa wakivuka Mto Miombo huku vijana sita wakidaiwa kuhusika na tukio hilo lililotokea katika Kijiji cha Mkata wilayani Kilosa mkoani hapa.

Tukio hilo lilitokea Januari 28 wakati kijana wa Kimasai, Baraka Lipando na mwenzake, Omari Omari kutoka Kijiji cha Ngaite wilayani Mvomero kuvamiwa na walipokuwa wakichunga mifugo porini katika mpaka wa Kijiji cha Ngaite na Mkata.

Baraka Lipando alisema walivamiwa na kundi la vijana sita wenye silaha za jadi na walipoona usalama wao ni mdogo walikimbia eneo hilo na kuiacha mifugo.

Baraka alisema baada ya kukimbia walipanda juu ya mti na watu hao wakaondoka na ng'ombe 84 waliokuwa wanawachunga na waliporejea nyumbani walitoa taarifa.

"Kundi la wale vijana walikuwa sita na mmoja wao tumemtambua kwa jina na sura na walikuwa na silaha za jadi wameshika mikononi," alisema Baraka.

Mmilikiwa wa mifugo hiyo, Mahamud Nasoro alisema kutokana na tukio hilo ng'ombe wake 16 wamekufa maji mtoni na wengine 45 hawajulikani walipo.

"Baada ya kusikia nilienda kutoa taarifa kituo cha polisi Doma na Januari 29 nilifika eneo la tukio na kuanza kufuatilia nyayo za mifugo na kuja kukuta ng'ombe 16 wamekuja maji. Ng'ombe 23 walirudi zizini wenyewe huku ng'ombe 45 hawajulikani walipo mpaka sasa," alisema Mahamud.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fourutunas Musilimu alisema Kituo cha Polisi Doma kilipokea taarifa ya ng'ombe kuporwa na 16 kufa maji huku ikimshikilia mtu mmoja kuhusiana na tukio hilo.

Kamanda Musilimu alisema tukio hilo lilitokea saa 12 jioni ya Januari 18 wakati Baraka Kipando na mwenzake, Omari wakichunga ng'ombe hao porini.

"Hawa wachunguji wameeleza kumtambua mmoja wa vijana hao sita kwa jina, Malisha Madirisha ambaye alionwa amebeba silaha nyeupe na wenzake watano wakiwa na fimbo mkononi baada ya kuona hivyo walikimbia na mbele walipanda juu ya mti kuwafutilia na kuwaona wakiondoka na ng'ombe hao kwenda kusikojulikana," alisema.

Kamanda Musilimu alisema siku moja baada ya tukio walienda kufuatilia nyayo za ng'ombe hao na kubaini baadhi walivuka mto lakini 16 walikutwa wamekufa maji mtoni.

"Kukamatwa kwa mmoja wa vijana wanaotuhumiwa kutasaidia kupatikana kwa wenzake. Jeshi la Polisi litahakikisha haki inatendeka kwani kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya imeshirikishwa ili kuondoa chuki, uhasama na migogoro, na matukio ya namna hiyo hayatakubalika,"alisema Kamanda Musilimu.

**MIGOGORO MOROGORO**

**Mkoa wa Morogoro ni kati ya maeneo yenye migogoro mingi ya ardhi inayowahusisha wakulima na wafugaji au wafugaji na wawekezaji. Migogoro hii hasa ile ya wakulima na wafugaji, imewahi kusababisha maafa yakiwamo yaliyotokea mwaka 2016 kiasi cha Serikali kuunda tume yauchunguzi iliyoongozwa na Jaji Jacob Mwambegele wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Hata sasa, wizi wa mifugo unaendelea kuwasumbua wananchi.**



## Kwa Ufupi

### Pingo's Forum walaani waandishi kukamatwa hifadhini



**Moshi**. Mashirika yanayowatetea wafugaji, wawindaji wa asili na waokota matundapori (Pingo's Forum) yamelaani tkuzuiwa na kuhojiwa kwa wanahabari sita waliokwenda kwenye mkutano wa wananchi wa Kijiji cha Nainokanoka kilichopo ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Waandishi hao walizuiwa Februari 3 na polisi pamoja na askari wa wanyamapori walipokuwa wanatoka kwenye mkutano huo.

Mkurugenzi wa Pingo's Forum, Edward Porokwa amesema wanalaani ukiukwaji huo wa haki za binadamu kwani siyo unavunja Katiba ya Tanzania bali ni kinyume cha sheria za nchi hata za kimataifa.

"Tunalaani vitendo vya polisi na askari wa mamlaka kuingilia uhuru wa wafugaji kukusanyika. Kuwakamata waandishi ni mkakati usiofaa wa taasisi husika kuhakikisha umma

Scanned with CamScanner